JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

8 JUNI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

TAREHE 8 JUNI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt.Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Neema Msangi

Baada ya kusoma Dua Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walitoka nje.

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasiishwa Mezani:-

1) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu):-

   a. Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii Nchini kwa mwaka 2013/2014 (*The Annual Report of Scocial Security Regulatory for the Year 2013/2014).*

   b. Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii Nchini kwa Mwaka 2014/2015 (*The Annual Report of Social Security Regulatory Authority for the Year 2014/2015).*

2) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha:-

   a. Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2016/2017.

   b. Taarifa ya Sera ya Fedha kwa Kipindi cha Mwaka 2015/2016 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2016/2017.

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa;

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.324 – Mhe. Josephine Thabita Chagula

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Josephine Thabita Chagula

(ii) Mhe. Amina Nassoro Makilagi
(iii) Mhe. Hussein Nassor Amar

Swali Na.325 – Mhe. Raphael Masunga Chegeni [kny. Mhe. Suzan Peter Masele]
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Raphael Masunga Chegeni
(ii) Mhe. Stanslaus Shing'homa Mabula
(iii) Mhe. Mwanne Ismael Mchemba

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Swali Na.326 – Mhe. Yahaya Omary Massare
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Yahaya Omary Massare
(ii) Mhe. Victory Kilasile Mwambalaswa
(iii) Mhe.Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

Swali Na. 327 – Mhe. Abdallah Dadi Chikota
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Abdallah Dadi Chikota
(ii) Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu
(iii) Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
(iv) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Swali Na.328 – Mhe. Joseph George Kakunda[Kny. Mhe. Masoud Abdallah Salim]
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Mboni Muhaji Mhita
(ii) Mhe. Amina Saleh Mollel

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:
Swali Na.329 – Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
(ii) Mhe. Joseph Kizito Mhagama
(iii) Mhe. Shally Joseph Raymond

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:
Swali Na.330 – Mhe. Albert Ntabaliba Obama
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Albert N. Obama
(ii) Mhe. Boniphace Mwita Getere
(iii) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq
(iv) Mhe. Subira Khamis Mgalu

Swali Na.331 – Mhe. Margaret Simwanza Sitta
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Margaret Simwanza Sitta
(ii) Mhe. Juliana Daniel Shonza
(iii) Mhe. Richard Mganga Ndassa
(iv) Mhe. Issa Ali Mangungu

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:
Swali Na.332 – Mhe. Atashasta Justus Nditiye
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Atashasta Justus Nditiye
(ii) Mhe. Halima Abdallah Bulembo

Swali Na.333 – Mhe. Ignas Aloyce Malocha
Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ignas Aloyce Malocha
(ii) Mhe. Jitu Vrajlal Soni
(iii) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke
(iv) Mhe. Omary Mohamed Mchengerwa

IV. MATANGAZO:

1. Wageni wote waliokuwepo Ukumbini walitambulishwa.

2. Kamati ya Katiba na Sheria ilitangaziwa kukutana kwa Kikao saa 5.00. asubuhi. Naibu Spika alisema wafanye baada ya kusitisha Bunge.

3. Kamati ya PIC ilitangaziwa kukutana tarehe 9/6/2016 saa 5.00 asubuhi kwenye Ukumbi wa Hazina.

4. Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro aliwaomba Wabunge wa Mkoa huo kukutana baada ya kusitisha Bunge.

5. Wabunge wa Mkoa wa Njombe waliombwa kukutana Kantini baada ya kusitisha Bunge.

6. Tangazo kutoka Ofisi ya Bunge kwamba leo tarehe 8/6/2016 kutakuwa na Hotuba ya Bajeti hivyo Wabunge wazingatie orodha ya Wageni walioalikwa kusikiliza Hotuba hiyo na hivyo wageni wa Wabunge hawataruhusiwa kuingia kama hawakualikwa na wageni walioko gallery asubuhi, ifikapo saa 6.00 mchana watatakiwa kuondoka.

7. Mhe. Leonidas Gama – Mwenyekiti wa mchezo wa kuvuta kamba alitangaza kuwaomba Wabunge wanaotaka kujiunga na mchezo huo wajiorodheshe majina yao.

8. Naibu Spika aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa jana wakati Waziri akijibu Swali la Mhe. Oliver Daniel Semguruka alisema ni Mbunge wa Mwanza kitu ambacho ni kosa, yeye ni Mbunge wa Kagera. Hivyo Hansard irekebishe hilo.

V. MWONGOZO WA SPIKA

Mhe. Richard Philip Mbogo alisimama kuomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), 44(4), 45(3), 46 (3) na Katiba ya Nchi Ibara ya 63(3)(a) kwamba jana tarehe 7/6/2016 kiti kilimnyima nafasi ya maswali ya nyongeza kwa Swali na. 180 jambo lililosababisha Wananchi kukosa haki yao ya msingi ya kupata majibu sahihi. Pia alisema Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (TAMISEMI) huwa anajibu vizuri maswali hayo yasiyo chini ya Wizara yake, kwa nini Serikali haikupewa nafasi kujibu swali hilo na Je, Swali hilo linaweza kurudiwa ili kuwatendea haki Wananchi?

Naibu Spika alijibu kuwa Mwongozo huombwa kwa jambo lililotokea mapema leo sio jana. Pili, Kanuni ya 44 kuhusu maswali, imeweka utaratibu wa jinsi maswali yanavyotakiwa kuulizwa kwamba hayatazidi mangapi lakini haijasema kila swali la msingi liwe na maswali ya nyongeza mangapi.

Vile vile Naibu Spika alisema Jana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijibu kwa niaba. Pia ifahamike kuwa maswali yanayokubaliwa ni yale yatokanayo na swali la msingi na Waziri Mwenye dhamana pia. Hivyo kama swali halikujibiwa vizuri siyo kwa sababu ya Waziri aliyejibu siyo mwenye dhamana.

Aidha, Wabunge waspokubaliana na kiti katika maamuzi yake wanaweza kutumia kanuni ya (5) kupata fursa ya kutoa malalamiko yao.

VI. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

TANGAZO:

Wabunge wote wanataarifiwa kikao cha pamoja kesho saa 4.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

VII. KUSITISHA BUNGE:

Saa 6.05 Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni.

VIII. BUNGE KUREJEA:

Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na Mhe. Dkt. Tulia Ackson. Wabunge wa upinzani hawakuingia kabisa Ukumbini siku hii jioni.

IX. HOJA ZA SERIKALI:

Baada ya msafara wa Naibu Spika kuingia Ukumbini, Waziri wa Fedha na Mipango aliingia akiongozwa na Mpambe wa Bunge na alianza kusoma Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Baada ya kumaliza alitoa Hoja kuwa Bunge sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Bajeti hiyo.

X. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 12.00 Naibu Spika aliahirisha Bunge hadi tarehe 10/6/2016 saa 3.00 asubuhi.

DODOMA
8 JUNI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE